



TUME YA HAKI ZA BINADAMU NA UTAWALA BORA  
Kitalu Na. 339, Mtaa wa Nyerere - Kilimani  
S.L.P 4019, DODOMA  
Simu: +255 734 047 775; 734 119 978  
Barua Pepe: [info@chragg.go.tz](mailto:info@chragg.go.tz)  
Tovuti: [www.chragg.go.tz](http://www.chragg.go.tz)

---

Agosti 22, 2024

## **TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI**

### **Tamko la THBUB juu ya Kupotea kwa Watu Nchini**

---

Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora (THBUB) inapenda kuutaarifu umma kuwa, inaendelea kufanya chunguzi maalum za matukio ya kupotea kwa watu nchini kwa lengo la kubaini, pamoja na mambo mengine, chanzo na wahusika, na kutoa mapendekezo stahiki. Chunguzi hizo zinazoendelea kwa sasa zinahusisha mikoa ifuatayo Dar es Salaam, Singida, Mara, Shinyanga, Mwanza, Kagera, Geita, Kigoma, Tanga, Mbeya, Iringa, Kilimanjaro, Arusha, Ruvuma na Rukwa. Hatua hii ni mwendelezo wa chunguzi zinazohusu matukio ya kupotea kwa watu ambayo THBUB imekuwa ikiyafanyia kazi katika nyakati tofauti na taarifa zake kufikishwa katika vyombo vinavyohusika.

Katika taarifa kwa umma iliyotolewa na THBUB tarehe 19 Julai, 2024 ilieleza kazi ilizokuwa imetekeleza katika kipindi cha mwaka wa fedha 2023/2024 hususan katika eneo la uchunguzi wa malalamiko ya wananchi kuhusu uvunjifu wa haki za binadamu na ukiukwaji wa misingi ya utawala bora. Katika taarifa hiyo pia THBUB ilielezea azma yake ya kufuatilia matukio ya kupotea kwa watu nchini. Katika kufanikisha lengo hilo, THBUB ilikuwa imekwishafanya hatua zifuatazo:

- Utambuzi wa matukio hayo kulingana na vyanzo mbalimbali vya taarifa;
- Uchambuzi wa matukio hayo kwa maana ya sehemu yalikotokea na watu waliokuwa wanadaiwa kuhusika;
- Kuandaa mpango kazi wa namna ya kufuatilia matukio hayo kwa kuzingatia mamlaka yake; na
- Kuendelea na chunguzi kuhusu matukio hayo.

THBUB inatekeleza jukumu hili chini ya Ibara ya 130(1)(b) na (c) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, 1977 na Kifungu cha 6(1)(b) cha Sheria ya Haki za Binadamu na Utawala Bora Sura ya 391.

THBUB inatoa shukurani kwa wananchi kwa ushirikiano wao na inawaomba waendeleo kutoa ushirikiano kwa kutoa taarifa kwa vyombo vinavyohusika zitakazoweza kukomeshwa kwa matukio hayo yenye taswira ya uvunjifu wa haki za binadamu pamoja na kuimarisha ulinzi wa haki ya kuishi.

Imetolewa na:

(IMESAINIWA )

.....

Mathew P.M. Mwaimu (Jaji Mstaafu)

**Mwenyekiti**

Agosti 22, 2024